TUAMBIE

JARIDA LA SAUTI ZA BIASHARA TANZANIA

MAZINGIRA MAGUMU YA KUFANYA BIASHARA YANAENDELEA KUZOOFISHA UKUAJI WA BIASHARA

Toleo Na. TUA/01 - Januari 2024.

TOLEO LA UTANGULIZI

MAZINGIRA YA BIASHARA

Kazi yetu ni kuhabarisha, kuchagiza na kutetea kupatikana kwa mazingira rafiki na wezeshi ya biashara Tanzania.

SEF INSURANCE AGENCY

Aina za Bima Tunazotoa

- Bima ya vyombo vya moto mfano - magari, pikipiki, bajaji, trekta, tela, boti, meli n.k.
- Bima za majanga yanayotokana na moto, mafuriko, matetemeko kwenye majengo ya makazi na biashara, mali n.k. mfano maduka, migahawa, hoteli, nyumba za kulala wageni, maghala,majengo ya ibada, viwanja vya michezo, nyumba za kuishi na osi.
- Bima dhidi ya wizi/uvunjaji kwenye nyumba, biashara n.k.
- Bima za miradi, ujenzi, mitambo, mashine, kusarisha mizigo/mazao/bidhaa/fedha na kusari ndani na nje ya nchi (mtu mmoja au kikundi)
- Bima za aina nyingine mbalimbali kadri ya mahitaji ya mteja.

HUDUMA ZA BIMA

- Wakala ya Bima kwa niaba ya Kampuni ya

PHOENIX ASSURANCE

- PATA
- KATA BIMA
- BIMA SASA!!!

Mbeya:

Tupo Eneo la Sokoine

Wasiliana nasi kwa namba +255 753 383 000, +255 683 744 984

-Karibu ukate Bima SEF Insurance Agency ili tukukinge na kukudia pale ajali au majanga yanapotokea-

BAOBAB

SHULE BORA NA ZA KISASA KWA ELIMU

Shule zenye kutoa elimu bora yenye ufaulu, mazingira mazuri ya kujisomea, michezo, kujifunza stadi za maisha, fulsa za kutembelea vivutio vya utalii na yenye kujali afya ya mwanafunzi.

Mlete mwanao sekondari kwa kidato cha 5 na 6, kuna michepuo ya PCB, PCM,PGM, CBG, EGM, ECA, HGE, HKL, HGL na HGK.

Shule zipo kata ya mapinga pembezoni mwa barabara iendayo Bagamoyo.

Fomu za kujiunga na shule zinapatikana kwenye tovuti ya shule: *www.baobab.ac.tz* na *www.schools.co.tz.* Unaweza kutuma maombi kwa njia ya mtandao.

Kwa maelezo zaidi piga simu:

Awali & Msingi: +255 659 984 443
+255 659 984 448

Sekondari:

+255 739 611 539 / 0715 611 538
+255 762 611 538 / 0763 367 567

YALIYOMO

1. Changamoto tunazoziishi wafanyabiashara Tanzania (Uk 3)
2. Sauti za wafanyabiashara (Uk 4)
3. Uchambuzi wa nafasi ya Tanzania kushika nafasi ya 141 (5 & 6)
4. Mfanyabiashara wa mwezi (Uk 7)
5. Waraka wa mazingira ya kufanya biashara (Uk 8)
6. Makala: Mazingira ya biashara na urahisi wa kufanya biashara (Uk 9)
7. Elimu ya Fedha - Umuhimu wa akaunti ya Benki kwa mfanyabiashara (Uk 10)

UNGA MKONO KUPATIKANA KWA MAZINGIRA RAFIKI NA WEZESHI YA BIASHARA TANZANIA KWA KUDHAMINI AU KUTANGAZA NA JARIDA HILI

SALAMU TOKA TUAMBIE

Tunayofuraha kubwa kuwatumikia watanzania kupitia Jarida la **TUAMBIE** ikiwa ni njia ya kuongeza nguvu katika kuchagiza kupatikana kwa mazingira rafiki na wezeshi ya biashara katika nchi yetu ili kuongeza ajira, kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, kaya na taifa kwa ujumla na kuondokana na umasikini. Toleo hili la kwanza linalenga kutambulisha Jarida, aina ya maudhui, dhana na jukumu la Jarida. Tunaomba ushirikiano toka kwa wasomaji wetu, wafanyabiashara, Jumuiya za wafanyabiashara na taasisi zenye kusaidia jitihada kupatikina kwa mazingira rahisi ya kufanya biashara ili tuweze kufanya kwa kazi ya kupaza sauti na kuchagiza kupatikana kwa mazingira rafiki na wezeshi ya biashara kuwa rahisi na endelevu.

TIMU TUAMBIE

Mkurugenzi Mtendaji: Joel Mwakitalu; Mhariri: Richard Magambo; Waandaji: Patrick Daud & Simon Mwang'onda; Mhakiki wa Maandishi & Lugha: Juliana Mashindano; Afisa Masoko: Salehe Munisi na Noel Joel.

HABARI ZIJAZO FEBRUARI 2024

- Urasimu wa huduma za umma unavyodhoofisha Biashara.
- Dondoo za mazingira ya biashara ya kilimo cha mazao ya mimea.

UHAKIKA WA JARIDA LA TUAMBIE

- Jarida huwafikia walengwa wa changamoto husika.
- Waraka wa mazingira ya biashara huwafikia watatuzi wa changamoto ofisini kwao.



Joel Mwakitalu
Mkurugenzi Mtendaji

KUSEMEA CHANGAMOTO ZA BIASHARA

Endapo shirikisho au Jumuiya yaa wafanyabiashara inahitaji Jarida kufanyia kazi changamoto zao za mazingira ya biashara wasiliana nasi kwa baruapepe ili kuweka nafasi (booking) na kutuwezesha kufanya maandalizi sahihi.

Jarida hili hutoka kila baada ya miezi miwili na huandaliwa na
JM Media Group, S.L.P 42747 Dar es Salaam, simu: +255 713702841/784810010
baruapepe: info@jmmedia.co.tz

CHANGAMOTO TUNAZOZIISHI WAFANYABIASHARA TANZANIA

Kodi, tozo, ushuru juu, faini holela, vibali lukuki, amri na matamko kwa kila mwenye mamlaka, barabarani kumejaa utitiri wa askari (traffic) kila mmoja kupiga mkono kwa nafasi yake, hakuna anaejali muda, huwezi kuwahi popote, gharama za biashara zinaongezeka, faini za traffic zimegeuka kuwa chanzo cha mapato cha kutegemewa badala ya kuwa adhabu.

Unalipa kodi kabla hujaanza kufanya biashara, unapoanza biashara hupati hati huru ya kodi (tax clearance) hadi ulipe kodi ya makadirio ya mapato na kodi ya pango la chumba cha biashara (mtu huyu hajaanza biashara ili kuigiza mapato, anapata wapi mapato ya kulipia kodi? – huu ndio mwazo wa rushwa). Mizunguko kwenye taasisi za vibali hadi uzeeke, petroli haishikiki, umeme bei juu na wenye kukatika mara kwa mara, unalazimika kuwa na Tanesco yako (Generator), rushwa sio neno zuri (sema uwezeshaji) imeanza kuwa sehemu ya gharama za huduma la sivyo huendi hatua ya pili, vikwazo kwenye kila hatua.

Kusafirisha mizigo kutoka bandarini Dar es Salaam hadi ufike Kimara inatakuchukua masaa 2 au 3 kisa foleni barabara ya mandela. Ukiwa unaendesha loli barabara za Tanzania basi ujue kuwa Traffic ni sehemu ya gari lako, jipange sawasawa lasivyo utakesha barabarani, kila hatua utapigwa mkono, ukibishana nao utambiwa unamzuia askari kutekeleza majukumu yake, hapo utakuwa umezua kosa gumu zaidi, utaishia kituoni.

Shamba umelima mwenyewe mahitaji yako na kwa nguvu zako kuuza soko la nje ya nchi unahitaji kibali, makatazo ya uuzaji wa nafaka soko la nje ya nchi umekuwa ndio mkakati wa hakikisho la usalama wa chakula kwa

Traffic kila eneo

Kukatikatika kwa umeme

Miundombinu ya barabara ni mibovu

hasara ya Mkulima. Je, hakuna fikra tofauti zaidi ya katazo la kuuza nje?? Kwa mtindo huu umasikini hautatutoka...

Tukipiga kelele itaundwa tume hata kama suluhisho linajulikana, tunapewa ahadi zisizo za kisheria sawa na mgonjwa kupewa Panadol, hakuna kinachobadilika......... ugonjwa utaendelea... Kila kona ni maumivu kwa mfanyabiashara.........

Pamoja na serikali kufanyia kazi utatuzi wa baadhi ya changamoto ukweli ni kuwa bado mazingira ya kufanya biashara sio rafiki, hasa kwa biashara ndogo na mpya. Vikwazo vipya vinazalishwa na mamlaka mbalimbali.

Ili Tuweze Kutoka Hapa Tunahitaji Mabadiliko Makubwa ya Kifikra, Kimtazamo, Maarifa, Utashi wa Kisiasa na Matendo.

SAUTI ZA WAFANYABIASHARA

Katika mahojiano na wafanyabiashara wadogo na wakati katika Jijini Dar es Salaam walieleza changamoto ambazo ufumbuzi wake umekuwa bado ni kitendawili, baadhi ya changamoto hizo ziko katika maeneo yafuatayo:

Leseni za Biashara Manispaa/Halmashauri kwa Mfumo wa TAUSI

Mfumo wa leseni wa TAUSI uzuri wake unaathiriwa na kukosekana kwa umadhubuti/uimara wake, mara kwa mara mfumo haufanyi kazi au unahitilafu wakati mwingine wiki 1 hadi 2 mtu anasubiri kupata leseni na hivyo kusimamisha biashara kwa kuwa bado hajapata leseni. Je, wahusika wa mfumo wa TAUSI wanajua hasara ya kibiashara na mapato ya serikali inayotokana na mfumo kutofanya kazi? Wizara inayosimamia halmashauri na manispaa inahitaji kufanyia kazi kwa makusudi kero hii ili kuokoa upotevu wa mapato ya serikali kwa biashara kutofanya kazi.

Kulipa Kodi Unapoanza Biashara

Kwa mtu anayeanza kufanya biashara kuanza kulipa kodi ikiwa pamoja na ushuru wa kodi ya pango la chumba cha biashara kabla hajaanza kufanya biashara yenyewe hii ni changamoto nzito kwa wengi na hasa wenye mitaji midogo; hili linachangia wengi kukwama kibiashara. Wizara ya fedha nini kinazuia nafuu ya biashara ndogo kutolipa kodi hadi baada ya miezi sita kuwa sehemu ya sheria ya kodi badala ya kuwa maagizo ya kisiasa yasiyo na nguvu ya sheria?

Wingi wa Traffic Barabarani na Faini Zake

Idadi ya traffic barabarani inazidi kuongezeka kila kukicha, karibu kila barabara kuna makundi ya traffic, tunasimamishwa sana na hivyo kupoteza muda mrefu kiasi cha kuathiri biashara na mapato yetu, gharama za barabarani zimezidi kuwa kubwa. Faini za mashine zimepitiliza kiasi cha kuanza kuzoeleka kuwa ni gharama za barabarini ukiwa na chombo cha moto, maonyo mengine na kuelimishwa kwa makosa madogo yamefutwa na ujio wa mashine. Ukisimamishwa ujue ni faini tu... Kwa wakuu wa kitengo cha traffic, hivi hakuna njia na teknolojia nyingine inayoweza kutumika iliyo bora zaidi badala ya kujaza idadi ya traffic barabarani?

Leseni za Usafirishaji LATRA

Mtandao kutokuwa imara - kukosekana mara kwa mara imekuwa ni usumbufu mkubwa wakati mwingine unaweza kusubiri siku 2 hadi 3 kusajili gari/chombo au kupata leseni. Faini 250,000 dereva mwingine kuendesha gari endepo wa awali aliyesajiliwa na gari hayupo hili ni janga jipya kwa uhalisia wa biashara ya Daladala. Je, wahusika na mtando wa LATRA wanajua hasara ya biashara na mapato ya serikali inayotokana na mtandao kutofanyakazi mara kwa mara?

Ushuru wa Kutumia Vituo wa Daladala kwa Manispaa

Ushuru ya maegesho kituoni ni 2,000 kila siku kwa basi moja, ukichelewa kukata asubuhi faini yake ni Tshs 250,000, ukubwa wa faini hauendeni na ukubwa wa kosa wala uhalisia wa biashara. Tunaumizwa sana. Manispaa zinahitaji kuimarisha njia za kuvutia na rafiki kwa Daladala ili kuongeza mapato badala ya kuja na njia zinazoua biashara zao na hivyo kukosa mapato zaidi ya kuwanufaisha watu wachache.

Bima kwa Bajaj na Pikipiki - Bodaboda

Kampuni nyingi za Bima hazipendelei kufanya biashara ya Bima na Bajaj na Bodaboda (Pikipiki za biashara) kwa hoja kuwa wana ajali nyingi. Hivyo endapo umekata bima ukipata ajali, urasimu wake wa kudai fidia ni bora ujichange mwenyewe, hivyo kwetu Bima ni hasara nyingine. Je, Mamlaka ya BIMA inatambua kero hii ambayo inadhoofisha maana na ukuaji wa Bima na hasa ukitambua kuwa Bodaboda na Bajaj zimeajiri watu wengi ambao pia ni walipa kodi?

KANUSHO (Disclaimer): Habari zilizoandikwa juu ya changamoto na sauti za wafanyabiashara ni maelezo ya wadau waliohojiwa, si maelezo au mawazo ya Jarida la Tuambie au JM Media, hivyo Jarida halihusiki maelezo hayo wala haitahusika na madai yoyote juu ya habari hizo..

UCHAMBUZI WA TANZANIA KUSHIKA NAFASI YA 141 KWENYE URAHISI WA MAZINGIRA YA BIASHARA DUNIANI 2019

Kwa miaka zaidi ya 17 Benki ya Dunia imekuwa inafanya zoezi la kupima mazingira ya biashara kwa nchi karibu 190 duniani ili kuchagiza kupatikana kwa mazingira bora ya biashara duniani ili kukuza uchumi wa dunia na kupunguza umasikini.

TABLE 0.1 Ease of doing business ranking

Rank	Economy	DB score	Rank	Economy	DB score	Rank	Economy	DB score
1	New Zealand	86.8	65	Puerto Rico (U.S.)	70.1	128	Barbados	57.9
2	Singapore	86.2	66	Brunei Darussalam	70.1	129	Ecuador	57.7
3	Hong Kong SAR, China	85.3	67	Colombia	70.1	130	St. Vincent and the Grenadines	57.1
4	Denmark	85.3	68	Oman	70.0	131	Nigeria	56.9
5	Korea, Rep.	84.0	69	Uzbekistan	69.9	132	Niger	56.8
6	United States	84.0	70	Vietnam	69.8	133	Honduras	56.3
7	Georgia	83.7	71	Jamaica	69.7	134	Guyana	55.5
8	United Kingdom	83.5	72	Luxembourg	69.6	135	Belize	55.5
9	Norway	82.6	73	Indonesia	69.6	136	Solomon Islands	55.3
10	Sweden	82.0	74	Costa Rica	69.2	137	Cabo Verde	55.0
11	Lithuania	81.6	75	Jordan	69.0	138	Mozambique	55.0
12	Malaysia	81.5	76	Peru	68.7	139	St. Kitts and Nevis	54.6
13	Mauritius	81.5	77	Qatar	68.7	140	Zimbabwe	54.5
14	Australia	81.2	78	Tunisia	68.7	141	Tanzania	54.5
15	Taiwan, China	80.9	79	Greece	68.4	142	Nicaragua	54.4
16	United Arab Emirates	80.9	80	Kyrgyz Republic	67.8	143	Lebanon	54.3
17	North Macedonia	80.7	81	Mongolia	67.8	144	Cambodia	53.8
18	Estonia	80.6	82	Albania	67.7	145	Palau	53.7
19	Latvia	80.3	83	Kuwait	67.4	146	Grenada	53.4
20	Finland	80.2	84	South Africa	67.0	147	Maldives	53.3
21	Thailand	80.1	85	Zambia	66.9	148	Mali	52.9
22	Germany	79.7	86	Panama	66.6	149	Benin	52.4
23	Canada	79.6	87	Botswana	66.2	150	Bolivia	51.7
24	Ireland	79.6	88	Malta	66.1	151	Burkina Faso	51.4
25	Kazakhstan	79.6	89	Bhutan	66.0	152	Mauritania	51.1
26	Iceland	79.0	90	Bosnia and Herzegovina	65.4	153	Marshall Islands	50.9
27	Austria	78.7	91	El Salvador	65.3	154	Lao PDR	50.8
28	Russian Federation	78.2	92	San Marino	64.2	155	Gambia, The	50.3
29	Japan	78.0	93	St. Lucia	63.7	156	Guinea	49.4
30	Spain	77.9	94	Nepal	63.2	157	Algeria	48.6
31	China	77.9	95	Philippines	62.8	158	Micronesia, Fed. Sts.	48.1
32	France	76.8	96	Guatemala	62.6	159	Ethiopia	48.0
33	Turkey	76.8	97	Togo	62.3	160	Comoros	47.9
34	Azerbaijan	76.7	98	Samoa	62.1	161	Madagascar	47.7
35	Israel	76.7	99	Sri Lanka	61.8	162	Suriname	47.5
36	Switzerland	76.6	100	Seychelles	61.7	163	Sierra Leone	47.5
37	Slovenia	76.5	101	Uruguay	61.5	164	Kiribati	46.9
38	Rwanda	76.5	102	Fiji	61.5	165	Myanmar	46.8
39	Portugal	76.5	103	Tonga	61.4	166	Burundi	46.8
40	Poland	76.4	104	Namibia	61.4	167	Cameroon	46.1
41	Czech Republic	76.3	105	Trinidad and Tobago	61.3	168	Bangladesh	45.0
42	Netherlands	76.1	106	Tajikistan	61.3	169	Gabon	45.0
43	Bahrain	76.0	107	Vanuatu	61.1	170	São Tomé and Príncipe	45.0
44	Serbia	75.7	108	Pakistan	61.0	171	Sudan	44.8
45	Slovak Republic	75.6	109	Malawi	60.9	172	Iraq	44.7
46	Belgium	75.0	110	Côte d'Ivoire	60.7	173	Afghanistan	44.1
47	Armenia	74.5	111	Dominica	60.5	174	Guinea-Bissau	43.2
48	Moldova	74.4	112	Djibouti	60.5	175	Liberia	43.2
49	Belarus	74.3	113	Antigua and Barbuda	60.3	176	Syrian Arab Republic	42.0
50	Montenegro	73.8	114	Egypt, Arab Rep.	60.1	177	Angola	41.3
51	Croatia	73.6	115	Dominican Republic	60.0	178	Equatorial Guinea	41.1
52	Hungary	73.4	116	Uganda	60.0	179	Haiti	40.7
53	Morocco	73.4	117	West Bank and Gaza	60.0	180	Congo, Rep.	39.5
54	Cyprus	73.4	118	Ghana	60.0	181	Timor-Leste	39.4
55	Romania	73.3	119	Bahamas, The	59.9	182	Chad	36.9
56	Kenya	73.2	120	Papua New Guinea	59.8	183	Congo, Dem. Rep.	36.2
57	Kosovo	73.2	121	Eswatini	59.5	184	Central African Republic	35.6
58	Italy	72.9	122	Lesotho	59.4	185	South Sudan	34.6
59	Chile	72.6	123	Senegal	59.3	186	Libya	32.7
60	Mexico	72.4	124	Brazil	59.1	187	Yemen, Rep.	31.8
61	Bulgaria	72.0	125	Paraguay	59.1	188	Venezuela, RB	30.2
62	Saudi Arabia	71.6	126	Argentina	59.0	189	Eritrea	21.6
63	India	71.0	127	Iran, Islamic Rep.	58.5	190	Somalia	20.0
64	Ukraine	70.2						

Mwaka 2019 Tanzania ilishika nafasi ya 141 kati ya nchi 190 ikiwa ni kurudi nyuma kwa alama 9 kwani mwaka 2016 ilishika nafasi ya 132. Kwa kushika ya nafasi ya 141 tukiwa nyuma karibu kwa nchi zote majirani zetu ni kuwa nchi yetu ni dhaifu katika kuvutia mitaji na uwekezaji duniani. Pia nguvu zetu za kiuchumi ni ndogo kuweza kushindana kwenye uchumi wa kimataifa na wa kikanda kama zilivyo nchi zilizotuzidi.

Mazingira ya kufanya biashara yanapokuwa hasi au mabaya maana yake ni kuwa nchi inapoteza fursa nyingi za kiuchumi kwani watu wake hawawezi kutumia rasilimali zao kujilietea maendeleo ipasavyo na hivyo kupelekea kuongezeka kwa ukosefu wa ajira hatimae umasikini.

Nafasi za nchi jirani: Rwanda (38), Kenya (56), Uganda (116), Burundi (166), Congo DRC (183), Sudani Kusini (185), Zambia (85), Malawi (109), Msumbiji (138).

Tanzania ilikuwa haifanyi vizuri kwenye maeneo yafuatayo:

i. Utawala wa kodi
ii. Usajili wa mali
iii. Kuwakinga wafanyabiashara wadogo ambao wengi ni dhaifu kibiashara.
iv. Biashara mipakani
v. Vibali vya ujenzi
vi. Utaratibu wa kufilisika
vii. Kufungua na kufunga biashara.

Kutokana na kuwa taarifa za mazingira ya biashara zimekuwa hazitolewi kwa umma imekuwa vigumu kwa umma kujua kama kuna mabadiliko au hakuna japo uhalisia kwenye kufanya biashara unaonyesha kuendelea kuwepo kwa ugumu kufanya biashara kutokana na mazingira magumu, yenye chuki, vitisho na yasiyotabirika. Katika baadhi ya maeneo au biashara mazingira ya kufanya biashara yamezidi kuwa magumu na yenye changamoto nyingi zinazohatarisha uhai wa biashara nyingi.

Ushahidi mzuri juu ya biashara nyingi kufa ni ule wa BRELA kufuta Kampuni za biashara takribani 5200 mwaka 2022 kwa kuwa hazikuwa hai kwa mujibu wa taratibu za BRELA. Kutokana na kushika nafasi ya 141 kati ya nchi 190 yapo maswali mengi ya kujiuliza kwa mfano:

Je, tunawezaje kuvutia uwekezaji mkubwa ili kutoa ajira nyingi kwa watu wetu wakati mazingira ya biashara nchini kwetu sio rafiki? Mtandao mmoja wa Marekani uliandika ifuatavyo juu ya mazingira ya biashara Tanzania. *"Among the major challenges U.S. firms experience in doing business in Tanzania include bureaucracy, corruption, and underdeveloped infrastructure. There is a slow pace of decision making at various levels creating room for corruption to fast track one's request".* Hivi ndivyo kampuni za kimataifa tunazozialika kuwekeza kwetu zinavyotutathimini. Je, katika hali hiyo tutatoka kweli endapo hakuna mabadiliko ya makusudi na ya dhati?

Je, tunawezaje kuajiri vijana wengi wanaomaliza vyuo kupitia biashara ikiwa mazingira ya ufanyaji biashara sio rafiki? Ndio maana ajira kwa vijana bado ni kitendawili.

Je, tunawezezaje kuongeza mapato ya kodi na ushuru endapo biashara nyingi zinakufa (kodi nazo hufa) au kuongeza idadi ya walipa kodi wakati wanaoanzisha biashara mpya ni wachache sana? Mzigo wa kodi unabaki kuwaangukia wafanyabiashara wachache.

Historia yetu ya Ujamaa kwenye mtazamo wa biashara kisiasa na utamaduni bado inatutafuna, mtazamo, wetu wa kisiasa na kiutamaduni juu ya biashara bado ni hasi, tena wengine wana chuki kubwa na wafanyabiashara. Kufanya biashara bado kunaonekana ni jambo baya au dhambi na lenye kuleta mashaka na hivyo kupelekea kutofurahiwa na kutokukubalika na wenye ufunguo wa mazingira rafiki ya biashara. Bado wapo watendaji na viongozi wa serikali na wa kisiasa ambao hawana mtazamo chanya na sekta binafsi, bado wanaamini katika uchumi wa serikali kufanya au kuendesha shughuli zote ikiwemo biashara. Baadhi ya watendaji na viongozi hao ndio wamepewa jukumu la kuleta mageuzi ya mazingira ya biashara. Je, watafanya tofauti na mtazamo wao? Ndio maana mageuzi ya mazingira ya biashara nchini hayaendi kwa kasi inayostahili. Wanaoukaba koo mkakati wa mageuzi ya mazingira ya kufanya biashara wako ndani ya serikali yenyewe

Serikali na Bunge wanapaswa kuweka mfumo wa kisheria kulinda na kuzuia kuondolewa kwa mafanikio ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuepuka kurudi nyuma kama ilivyotokea kati ya mwaka 2017 na 2020.

Swali: Je, nini kifanyike ili kubadili mtazamo wa waandaji, watungaji, watekelezaji na wasimamizi wa sera, sheria, kanuni na taratibu juu ya biashara na sekta binafsi?

Endapo una majibu au ushauri juu ya swali hilo, tuandikie kwa baruapepe:

tuambietz@gmail.com

Uchambuzi umefanywa na Joel Mwakitalu
Mtaalamu wa Maendeleo ya Biashara

MFANYABIASHARA WA MWEZI JANUARI

GABRIEL JULIUS MGETA
Mkurugenzi Mtendaji

Umri wa Kampuni Kwenye Biashara
Miaka 10

Biashara Kuu Zinazofanywa
Ukaguzi wa Hesabu

Aina ya Huduma Zinazotolewa
Uandaaji wa hesabu, ukaguzi wa hesabu, ushauri wa kodi.

Sifa Kuu za Kampuni
Huduma nzuri zinazozingatia muda kwa gharama nafuu.

Matarajio ya Kampuni Kibiashara Kuendelea
kuwahudumia wateja wadogo, wa kati na wakubwa.

Ahadi za Kibiashara za Kampuni
Kwa Wateja
Lumbika tutaendelea kutoa huduma bora, kwa wakati na kwa gharama nafuu.

LUMBIKA
Tanzania

Mahali Tulipo na Mawasiliano
Mezzanine Floor, Victoria Place, New Bagamoyo Road, Kijitonyama
P. O. Box 100255, Dar Es Salaam
Simu: +255 735 000 127
+255 714 290 649
Email: info@lumbika.co.tz
Tovuti: www.lumbika.co.tz

Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu

Ukitaka kuwa mfanyabiashara wa mwezi, tuandikie uweze kujua vigezo na masharti
Baruapepe: tuambietz@gmail.com

WARAKA WA MAZINGIRA YA BIASHARA

Kwa Waziri Mwenye Dhamana ya Kusimamia Biashara Tanzania
Agenda: Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara

Mheshimiwa Waziri,

TUAMBIE tunapenda kukupongeza kwa kuaminiwa na Raisi wetu kuwa wewe unaweza kusimamia mageuzi na maendeleo ya sekta ya biashara katika taifa letu. Hongera sana.

Ni imani yetu pia kuwa wizara yako ndio nguzo na mratibu wa mikakati inayohusu mageuzi katika mazingira ya kufanya biashara nchini kupitia mkakati (blue print) wa serikali wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara wa mwaka 2018. Kwetu sisi wafanyabiashara wewe na wizara yako umebeba mzigo wa matumaini ya watanzania juu ya kuboresha maisha yao kupitia biashara zao. Hivyo kipimo cha wafanyabiashara wa Tanzania juu yako na wizara yako ya Biashara ni mabadiliko chanya kwenye mazingira ya kufanya biashara.

Mwezi Novemba 2023 tulisoma habari juu ya wenyeviti wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) wakieleza juu ya mafanikio ya kupungua kwa tozo, faini, kodi, sheria, kanuni na taratibu kero za biashara. Bahati mbaya hizo kero tozo, kodi na sheria, kanuni na taratibu zilizoelezwa kufanyiwa marekebisho au kuondolewa hazikutajwa kwa hiyo kwa mfanyabiashara ambaye maneno bila ushahidi ulio wazi kwenye uhalisia wa biashara kujulikana hakumsaidii; kilichotakiwa ni kuzitaja na kuziorodhesha kwenye magazeti ili kila mtu azijue ili aweze kuthibitisha kiuhalisia kwenye kufanya biashara. Kwa mantiki hiyo tunapenda kuwasilisha ushauri wetu juu ya mkakati uliopo wa kuboresha mazingira ya biashara nchini:

1. Mkakati uwekwe wazi kwa umma; umma ndio unaofanya biashara na uwe kwa lugha ya Kiswahili kwa yale mambo muhimu kwa umma kuyajua, kuyatekeleza na kuyafuatilia.
2. Uwekwe utaratibu wa wizara ya Biashara kuchapisha kwenye magazeti sheria, kanuni, taratibu, kodi au tozo zilizofanyiwa marekebisho au kuondolewa pale marekebisho yanapofanywa.
3. Ifanywe tathimini juu ya utekelezaji wa mkakati/mpango toka mwaka 2019 hadi 2023 na matokeo yake yawekwe hadharani kwa wananchi.
4. Uwekwe utaratibu endelevu wa kupima na kutoa tathimini ya utekelezaji wa mkakati huo kila mwaka kwa umma kupitia magazeti, radio na televisheni. Utaratibu ushirikishe umma katika kupima matokeo.
5. Uwekwe utaratibu rahisi wa umma kushirikishwa kutoa mawazo tofauti na yale ya wataalamu au serikali juu ya mkakati wa kuboresha mazingira ya biashara.

Mtazamo Wetu

Biashara yoyote, iwe inafanywa na taasisi ya umma au ya binafsi inahitaji mazingira rafiki na wezeshi ya kufanya biashara ili iweze kukua, kuendelea na kuwa na tija.

Tunakushukuru na kukutakia mafanikio katika kuwatumikia watanzania.

Mungu Ibariki Tanzania!! KAZI IENDELEE!!

Mhariri

MAZINGIRA YA BIASHARA NA URAHISI WA KUFANYA BIASHARA

Makala Na. 1

Dhana ya Mazingira ya Biashara

Mazingira ya Biashara ni mambo ambayo uwepo wake au kokesekana kwake kunawezesha biashara kufanya vizuri au vibaya. Kwa mtazamo chanya mbao ndio unaotarajiwa na mtu au watu wanapoamua kuingia kufanya biashara ni kuwa wanatarajia kuwa mazingira ya biashara yatakuwa ni rafiki na wezeshi kwa biashara kufanya vizuri yaani kukua na kupata faida iliyoendelevu.

Nafasi ya Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu Katika Biashara

Kwa sehemu kubwa mazingira ya Biashara hujengwa na sera, sheria na kanuni za nchi, au eneo au mataifa. Sera huzaa sheria, sheria huzaa kanuni huzaa taratibu za utekelezaji ambazo biashara hutumia kuingia kwenye biashara, kufanya biashara na kuondoka kwenye biashara. Urahisi wa kufanya biashara katika eneo, nchi au kimataifa hutegemea sana hali ya sera, sheria na kanuni zinazotawala aina ya biashara. Viwango vya kodi, ushuru, tozo, na urasimu kupata vibali hutokana na sera, sheria na kanuni. Unaposikia malalamiko ya wafanyabiashara juu ya jambo fulani na hasa kodi, ushuru, tozo na urasimu katika utaratibu wa kupata vibali au kupata hati au haki fulani basi ujue kuwa kuna jambo katika sera au sheria au kanuni au taratibu za utekelezaji sio rafiki na wezeshi kwa biashara. Ndio maana ni muhimu sana kwa wafanyabiashara kujua sera, sheria, kanuni na taratibu zinaongoza biashara zao ili waweze kutambua haki zao na vilevile waweze kutambua tatizo au changamoto inayowakabili ili waweze kulisema tatizo au changamoto hiyo kwa uhakika..

Ushauri

Katika kufanikisha nchi kuwa na mazingira rafiki na wezeshezi kwa biashara itakuwa ni kwa faida ya pande zote mbili yaani serikali na wafanyabiashara kwa serikali au idara au taasisi husika kuweka hadharani sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia biashara husika. Itafaa zaidi endapo kila wilaya kutakuwa na duka la machapisho ya serikali lenye kuuza sera, sheria, kanuni na taratibu za biashara mbalimbali. Hii itawezesha wafanyabiashara kufanya biashara kwa uelewa wa sera, sheria, kanuni na taratibu, pia itawezesha kufanya tathimini ya sera, sheria, kanuni na taratibu husika kwenye biashara kwa uhusiano wa moja kwa moja na wafanyabiashara.



Imeandaliwa na JM Media

ELIMU YA FEDHA

UMUHIMU WA AKAUNTI YA BENKI KWA MFANYA BIASHARA

Akaunti ya Benki ni Ushahidi wa Kufanya Biashara Rasmi

Katika ulimwengu wa sasa wa biashara, biashara zinatambulika kuwa rasmi kwa pale zinapofanya miamala ya biashara zake kupitia akaunti ya benki. Maana yake ni kuwa unatakiwa kufanya malipo, manunuzi au matumizi yako kupitia akaunti yako ya benki. Ukishakamilisha mauzo ya biashara yako ya siku ingiza mauzo ya siku benki na utoe mahitaji ya fedha zako kutoka benki. Taarifa ya benki (benki statement) ya akaunti yako ya biashara ndiyo itakuwa ushahidi sahihi kuwa wewe unafanya biashara iliyo rasmi. Unapohitaji kukopa ushahidi wa taarifa ya benki ya akaunti yako hutumika kama ushahidi rasmi. Taarifa ya akaunti yako ya biashara ya benki hutumika katika kuthibitisha biashara zako kuwa rasmi unapohitaji kupata wawekezaji au kuingia kwenye zabuni au kufanya biashara na kampuni kubwa.

Akaunti ya Benki ni Kielelezo cha Mzunguko Wako wa Kifedha

Kielelezo rasmi cha hali ya mzunguko wa kifedha katika biashara ni taarifa ya kibenki ya akaunti. Unapohitaji kukopa benki au kampuni za mikopo hutumia taarifa za kibenki za akaunti zako kutambua na kupima ukubwa wa mzunguko wa kifedha wa biashara zako. Hivyo unahitaji kutumia sana akaunti yako ya biashara ya benki kujijengea ushahidi wa uwezo wako kibiashara kupitia akaunti yako ya benki.

Akaunti ya Benki ni Ushahidi wa Uwezo Wako wa Kifedha Katika Biashara

Taarifa ya akaunti yako benki huonyesha uwezo wako wa kifedha kibiashara kwa maana ya mauzo, manunuzi au matumizi hujulikana kupitia akaunti ya benki na sio vinginevyo. Epuka au punguza kufanya malipo au manunuzi bila kupitia kwenye akaunti ya benki. Endapo unatumia fedha kwenye simu basi itakuwa na faida kwako kutumia njia ya "simbanking" ili uweze kuendelea kuitumia akaunti yako ya benki na hivyo kuimarisha taarifa zako za biashara kifedha kupitia akaunti ya benki.

Akaunti ya Benki ni Usalama Wako Kibiashara

Matukio ya kupoteza fedha tasilimu kwa kuporwa au kuibiwa yamekuwa mengi miongoni mwa wafanyabiashara hii inathibitisha umuhimu mfanyabiashara anayejitambua kutumia benki kufanya biashara zake kwa mantiki ya usalama wa fedha zake. Benki ndio mahali salama kwa fedha zako. Fungua akaunti ya biashara benki na uitumie.

Ushauri: Wafanyabiashara tuchukue hatua ya kutumia akaunti zetu za benki (akaunti za biashara) kikamilifu ili kujijengea ushahidi uliorasmi, unaoaminika, unaoweza kukusemea bila hata ya wewe kuwepo.

Imeandaliwa na: Joel Mwakitalu
Mshauri wa Elimu ya Fedha
0713 702 841

Makala ya Elimu ya Fedha imeletwa kwenu kwa uhisani wa SEF INSURANCE AGENY (Wakala wa Bima). Karibu upate huduma za Bima ukiwa Mbeya. Tupigie kwa simu namba 0753383000/0683744984

SEF INSURANCE AGENCY


HAPPY NATION
BUS BUSINESS CLASS
For reliable, secure, and comfortable services.
Enjoy Air-conditioning, free Wi-Fi internet, cinema, and soft drinks.
Daily Services From Dar es Salaam to:
Kahama, Bukoba, Mwanza, Shinyanga, Bariadi, Musoma, Mbeya, Tabora and Mpanda.
Book Online or contact us at:
+255 745 039 200
+255 745 083 665
+255 745 459 685
Visit our website: www.happynation.co.tz

Travel Partner®
KWA USAFIRI WA SALAMA NA UHAKIKA WA ABIRIA PAMOJA NA VIFURUSHI KWA MABASI YA STAREHE (LUXURY BUS)
USAFIRI WA MABASI KUTOKA DAR KWENDA:
DODOMA, SINGIDA, SHINYANGA, MWANZA, BUKOBA NA KARAGWE
KWA SAFARI NA USAFIRI WA UTALII
Tunaandaa safari na usafiri wa utalii kutembelea mbunga zote za wanyama Tanzania na maeneo mengine ya utalii. Pia tunakodisha magari madogo na mabasi kwa shughuli mbalimbali.
Wasilian nasi:
0767 888 382
0767 888 172
Au tembelea tovuti yetu: www.travelpartner.co.tz
-Karibu Usafiri na Utalii na Travel-